# UBAINIFU YAKINIFU

(kuhusu makosa ya kimanhaji na kielimu, yaliofanywa na baadhi ya wanaojinasibisha na maswala ya elimu)

## MAKALA NO (7)

**IMEANDIKWA NA**:

ABUU IBRAAHIIM IBNU AL IMAAM

٢٠/٤/١٤٣٨هـ

بسم الله الرحمن الرحيم.

الحمد لله رب العالمين، والصلاة والسلام على النبي الكريم، وعلى آله وأصحابه أجمعين.

أما بعد.

Baada ya kumshukuru Allah Mtukufu, na kumswalia Mtume wetu kipenzi, na Ahli zake, na Maswahaba wake wote:

**Ndugu msomaji,** baada ya kuona katika makala zilizopita makosa ya Abdurrah'maan katika matumizi ya neno Hizbu Llaah, na Waliyyu LLaah:

hatuna shaka kua tulichoongea katika mhadhara wa Masjid Al Amiin kuhusu ufafanuzi wa Hizbu Llaah na Hizbu Sshaitwaan ni sahihi kabisa, kwani tumefafanua kama walivyofafanua Ulamaa, na kama zilivyodalili.

Na kwa ufafanuzi huo (uliopita kwenye makala za nyuma) tunakuta jinsi Abdru Rrah'man alivyoingia kwenye makosa makubwa kama tulivyoona maneno yake huko nyuma, na pia kama unavyoona hapa alipokariri maneno yake ya kuwatoa wafanya maasi makubwa (miongoni waislamu) kwenye Hizbu ya

Allah ya ujumla pale **aliposema**:

"ni muhali katika pote la hizbu Llaah kupatikana maasi makubwa na bida'a"!

Tunamuambia Abdurrah'maan: usahihi ni kua: ni muhali kupatikana maasi makubwa na bida'a kwenye Hizbu Llaah na Mawalii wa Allah wenye maana na istilahi maalumu, nao ni wale walio na imani kamili kama tulivyoona sherehe za ulamaa.

Ama kupatikana watu wa bida'a na maasi makubwa kwenye Hizbu Llaah yenye maana ya ujumla, yani yenye maana ya waislamu wote dhidi ya makafiri: hili halina shaka kabisa kua wanapatikana kwa yale mema yao, na yale mabaya yao hayanasibishwi na Hizbu ya Allah!

Na hakuna shaka kua mtiririko uliyoongelewa kwenye aya, na kama walivyobainisha maulamaa, ni mtiririko unaoongelea waislamu kua ni Hizbu ya Alla, dhidi ya makafiri kua ni Hizbu ya shaitwaan, kwahiyo ilikua inaongelewa Hizbu Llaah ya maana ya

Ujumla na si maana khaaswa.

Lakini Abdrurrah'man alizidi kuchanganya madawa, na kuzidi kuharibu **pale aliposema**:(nanukuu maneno yake kama yalivyo):

"Ndani ya firqatu nnaajiya kuna uzushi? Ndani ya firqatu nnaajiya kuna makundi makundi? Hakuna, sasa huyu duktuur sijaelewa kwamba huu ufahamu wake kautoa kwa nani?"

Hivi unaelewa kweli? Hayo ni maneno kweli ya kielimu? Kwani shekhe Muqbili aliposema kwenye Tuhfatul Mujiib Uk 141 mpaka 142:

فحزب الرحمن لا يجوز لهم أن يتفرقوا

"Hizbu Llaah haijuzu kwao kufarikiana"

kisha akaleta aya na hadithi zinazokataza mapote, kama vile hadithi ya kukataza mapote sabini na tatu, na nk, alikusudia Firqatu nnaajiya? Hivi Firqatu nnaajiya ndio aliyokusudia Mtume Swalla Llaahu alaihi wasallam kua itagawanyika makundi sabini na tatu?

Hivi Firqatu Nnaajiya ndio iliyoitwa Umma kwenye hiyo hadithi? au uliongea kwa msukumo wa hasira na chuki?

Kisha maajabu mengine yaliyozidi kudhihirisha ufahamu usio sahihi wa Abdurrah'man katika mas'ala haya: ni pale alipo nukuu maneno ya Imaam Ibnu Baazi Rahimahu Llaah, **yasemayo:**

فكل طريقة أو عمل أو عبادة يحدثها الناس يتقربون بها إلى الله ويرونها عبادة ويبتغون بها الثواب وهي تخالف شرع الله فإنها تكون بدعة.

فتاوى نور على الدرب ص ١٨.

" kila njia au tendo au ibada ambayo wanaizusha watu, wakajikurubisha kwa Allah kwa hiyo Ibada na hayo matendo (waliyozua watu) na wakayaona kua ni Ibada, na wanataka thawabu kutokana na hayo waliyozusha, ambayo yanaenda kinyume na sheria ya Alla, hakika mambo hayo ni bida'a"

*Tazama: Fatawa nuurun ala ddarbi uk: 18.*

Baada ya (Abdurrah'maan) kunukuu maneno hayo akasema:

"Na sherehe ya sampuli kama hiyo ameitoa kwa nani? Al imaam Ibnu Baaz Rahmatu Llaahi alaihi akiisherehesha hadithi hii anasema maneno haya yafuatayo:

فكل طريقة أو عمل أو عبادة يحدثها الناس

Kila njia au matendo au ibada ambazo wanazusha watu, hakusema Hizbu Llaahi, hakusema:""yuhdithuhaa Hizbu Llaah" Hakusema ile ambayo wanazusha Hizbu llaah.

kwa sababu Hizbu Llaah ni kundi ambalo tayari wao wapo ndani ya sharia, tayari wao wapo vile mtume swalla llaahu alaihi wasallam na allah mtukufu anataka wawepo"

*Rejea kalima ya Abdurrah'man aliyoitoa ya kunijibu.*

## MAJIBU YA MANENO HAYO NI KAMA IFUATAVYO:

1- Ni jambo la kushangaza mtu kutoa ushahidi kama huu, kwa sababu maneno ya Shekhe (Allah amrehemu) hayana uhusiano kabisa na mada tunayojadili! Na hii inaonyesha kua huyu alikua anajibu bila kujiandaa!

2- kwa mujibu wa Abdru Rrah'maan hapo: wanaofanya madhambi makubwa miongoni mwa waislamu na watu wa bida'a kwa ujumla hawaingii

katika Hizbu ya Allah moja kwa moja, kwa sababu Imaam Ibnu baazi hakusema kua bida'a hizo zinazushwa na Hizbu Llaah, bali kasema zimezushwa na watu!

**Swali tunamuuliza**: mbona shekhe pia hakusema:

يحدثها المسلمون

"wanazizusha waislamu"?

Kwani ikiwa wao hawaingii kwenye kuitwa Hizbu Llaah moja kwa moja( yani hata kwa maana ya Ujumla) kwa mujibu wako, je vipi kuwaita waislamu? Na kwa kua Shekhe hajasema"wanazizusha waislamu" kwahiyo hawazingatii watu wa bida'a kua ni waislamu?

3- usahihi ni kua unaweza kuelezea waislamu wenye makosa kwa kutumia neno" baadhi ya waislamu wanafanya kadha, au wanazua kadha" na unaweza kutumia pia neno"watu" kwamba kuna watu wanafanya kadha, na kadha, na ukawa unawakusudia baadhi ya waislamu.

4- ufafanuzi unabaki ule ule tunaoukariri tangia mwanzo, kua wafanya bida'a na maasi miongoni mwa

waislamu wanaingia kwenye asli ya Hizbu ya Alla, kwamaana wanaingia kwenye kundi la Allah kwa ujumla, kulingana na asili ya imani zao na baadhi ya matendo yao mema, ikilinganishwa na makafiri.

Na watu hao hao wa bida'a na maasi hawaingii kwenye Hizbu ya Alla yenye maana maalumu iliokamilika, kwasababu ya kuzusha kwao, na ufasiki wao, na ndio maana huwezi kuwaita watu wa bida'a au wa maasia wanapopwekeka: "HIzbu LLaah au Waliyyu Llaah".

kwa sababu hiyo itakua na maana maalumu, na maana hiyo maalumu haiwi isipokua kwa Ahlussunna wenye kusimama kwenye twa'a.

Miongoni mwa maneno yanayoonyesha ufahamu usio sahihi wa Abdurrah'man katika mas'ala hii: ni kulazimisha ufahamu ambao haupo kwenye maneno yangu, kwa kudai kwake kua eti maneno yangu- kama ninavyomnukuu-:

"yanaonyesha kua Hizbu LLaah imegawanyika sehemu tatu, Hizbu LLaah ya Ujumla, Hizbu Llaah

Annaqiyyu(iliosafi) na Hizbu Llaah isiosafi"

**JAWABU:**

Kwa hakika huu ni ufahamu mwembamba sana! nilichoeleza ni kwamba: baada ya kuishi maswahaba na Mtume Swalla Llaahu alaihi wasallam bila kua na vikundi vikundi: zilikuja zama wakaingia watu wengi katika Uislamu kutoka maeneo mengi.

lakini kwa bahati mbaya baadhi ya watu hao walikuja kuzusha bida'a, na hivyo kutoka kwenye Kundi la Allah (Hizbu Llaah) iliokua safi na kusalimika na bida'a mbali mbali, na kua kwa kuanzisha kwao bida'a hizo:

wameingia kwenye orodha ya watu waliokemewa na Allah na kuahidiwa adhabu ya Allah kwa kadri ya viwango vyao vya bida'a.

Lakini pamoja na hivyo, hawatoki kwenye asili ya Hizbu Llaah, yani hawatoki kwenye asili ya imani, wanabaki katika Hizbu ya Allah kutokana na Asli ya

Imani yao na matendo yao mema, ikilinganishwa na makafiri (ukiondosha watu wa bida'a waliokufuru kwa kuzingatia misingi ya kisheria kwenye hilo).

**Kwamaana hiyo:** Hizbu Llaah inabaki kama tulivyofafanua huko juu, kua matumizi yake yako aina mbili kulingana na makusudio na mtiririko wa maudhui.

Ama hivi vigawanyo vitatu alivyotoa Abdurrah'man na kuviegemeza kwangu ni uzushi wa wazi!

Ama kuhusu kutoa dalili ya Qauli ya Allah katika suuratul An'aam aya ya 153 aliposema:

وأن هذه صراطي مستقيما فاتبعوه ولا تتبعوا السبل فتفرق بكم عن سبيله

" Na hakika hii ndio njia yangu iliyonyooka ifuateni, na msifuate vinjia vya pembeni mkafarikiana kwenye njia yangu"

Ambapo Mtume swalla llaahu alaihi wasallam aliifasiri aya hii kwa kuchora vinjia vya pembeni, na

kuchora njia moja kati kati iliyonyooka, kisha akasema: hii ndio njia ya Allah iliyonyooka, na hivi ni vijinjia vya pembeni, kila kijinjia kuna shetani anawaitia kwenye kinjia hicho.

Nikaeeleza kua hizo njia za pembeni zilizokatazwa kufuata, na ambazo kila njia ina shetani anaita watu, wanaingia ndani yake waislamu(watu wa bida'a na mafasiki) na wasio kua waislamu, na maneno niliyosema ni haya hapa:

" katika kila kijinjia katika hivyo vijinjia vya pembeni kuna shetani analingania watu, na katika hadithi, na shetani hapa anayekusudiwa wako waislam na wasiokua waislam kwa ushahidi wa hadithi ya nuumaan bin bashiir"

**Ambapo nataka kufafanua katika maneno haya mambo yafuatayo:**

1- Ni kweli nimeteleza kutaja jina la swahaba, badala ya kusema: Hudhaifatu Ibnul Yamaani nilitaja jina la Nu'umaan Bin Bashiir Radhi za Alla ziwaendee.

Na sikua nimetanabahi hilo isipokua baada ya

kuondoka kwenye muhadhara, ambapo baadae nilituma masahihisho ya baadhi ya makosa yaliyotokea kwenye Mhadhara huo likiwemo hilo kupitia grp moja la whatsApp liitwalo:

الدعوة السلفية في تنزانيا

Na Ilikua Tar: 15/8/2016 saa tano na dakika ishirini na tisa usiku, na niliamini kua Masahihisho hayo yalienea sehemu nyingi.

Maana grp hilo lilikua na watu zaidi ya mia moja, na nikawa nimeshaondosha Dhimma katika hilo, kama ambavyo wanafanya wanachuoni wetu wanapoteleza kwenye jambo hulirekebisha.

2- maneno haya niliyosema: "shetani hapa anayekusudiwa wako waislam na wasiokua waislam kwa ushahidi wa hadithi ya nuumaan bin bashiir(usahihi Hudhaifatu Ibnul yamaani)":

nilikusudia kua: Shetani aliyekusudiwa kwenye Aya ya Suuratul An'aam na Tafsiri yake kwenye Hadithi ya Ibnu mas'uud:

wako Waislam na wasiokua waislam, yani hiyo

Aya inayozungumzia vijinjia vinaingia vijinjinjia vya bida'a na dini batili.

Kisha nikasema: kwa ushahidi wa Hadithi (ambayo usahihi Imepokewa na Hudhaifa radhi za Alla zimuendee), ambayo imetaja walinganizi walioko kwenye milango ya motoni.

Lengo la kutaja hadithi hiyo: ilikua ni kutilia mkazo aya ya suuratul An'aam na Hadithi ya Ibnu Mas'uud radhi za Alla zimuendee wa kuingia baadhi ya waislamu kwenye vijinjia vya pembeni, na kuingia kwenye mashetani wanaolingania kwenye hivyo vijinjia!

Na lengo la kutaja hadithi hii ni kwa sababu iko wazi zaidi katika kuhusisha kuingia baadhi ya Waislamu(watu wa Bida'a) katika kuitia kwenye vijinjia vya pembeni, kuliko aya ya Suuratul An'aam na Hadithi ya Ibnu Ms'uud ambazo zinaonyesha kuingia waislam na wasio waislam.

Lakini kosa ambalo nimelifanya ni pale

niliposema:"shetani hapa anayekusudiwa wako waislam na wasiokua waislam kwa ushahidi" ambapo hilo neno:"kwa ushahidi" kwa haraka haraka linaleta maana kua natolea ushahidi wa hii hadithi kua wanaoongelewa kwenye hiyo hadithi ni waislamu(watu wa bida'a) na makafiri wa asili (mayahudi na manaswara).

Na katika kuiendea maana ambayo nilikua naielezea ilitakiwa niseme: "shetani hapa anayekusudiwa wako waislam na wasiokua waislam".

yani ilikua ni simame hapo, kisha nianze jumla nyingine inayojitegemea, kwa mafano ningesema:"na miongoni mwa ushahidi unaoonyesha kuingia baadhi ya waisalmu katika vijinjia vya pembeni: ni hadithi…."

**Kwa maana hiyo**: **Abdurrah'maan alikua ana haki ya kunikosoa kwenye hilo**, **lakini tatizo lake naye kaingia kwenye makosa kwenye ukosoaji wake**!

**Kosa la kwanza**: ni pale alipopinga kusema kwangu kuhusu aya ya suuratul An'aam kua

wanaolingania kwenye hivyo vijinjia vya pembeni wanaingia waislamu na wasiokua waislamu **ambapo amesema:**

" Kwamba: maneno haya ya kusema kwamba kila katika njia kuna shetani shetani ambaye wapo waislamu na wasiokua waislamu haya maneo umeyatoa wapi?"

## JAWABU LA MANENO HAYO NI KAMA IFUATAVYO:

Wanachuoni wamefasiri maana ya Assubulu (vijinjia) ambavyo shetani huitia kwa maana mbili.

**MAANA YA KWANZA**: wamesema: ni Dini za batili, kama uyahudi na unaswara.

**MAANA YA PILI**: wamesema: ni Bida'a na Matamanio.

Na si lazima tafsiri hizo ziwe ni khilafu, kwakua inawezekana maana zote mbili kutumika, na hilo ndilo tutakaloliona kwenye maneno ya wanachuoni yafuatayo:

1- Amesema Imaam wa wafasiri, Ibnu jariir **Attwabary** Rahimahu llaah, katika kufasiri neno la

Allah:

ولا تتبعوا السبل

"Na msifuate vijinjia" Amesema Attwabary:

يقول: ولا تسلكوا طريقًا سواه، ولا تركبوا منهجًا غيره، ولا تبغوا دينًا خلافه ، من اليهودية والنصرانية والمجوسية وعبادة الأوثان، وغير ذلك من الملل، فإنها بدع وضلالات"
تفسير الطبري ٢٢٩/١٢

" Anasema: na msipite njia isiokua (uislamu) na msipande manhaji isiokua hiyo,na msitafute dini kinyume chake, miongoni mwa dini za kiyahudi, na kinaswara, na kimajusi, na waabudu masanamu, na nyinginezo katika mila, hakika zote hizo ni bid'a na upotevu"

*Tazama: Tafsiri ya Ttwabari 12/229.*

2- Amesema Mwanachuoni Abul Mudhwaffar **Assam'aaniy** katika kuifasiri aya hiyo:

"ولا تتبعوا السبل " بمعنى : سائر الملل سوى ملة الإسلام وقيل : هو الأهواء والبدع.
تفسير السمعاني ١٥٧/٢

"Na msifuate vijinjia, maana yake (njia zilizokusudiwa): ni mila (dini) zote zisizokua uislamu, na imesemwa kua makusudio ya vinjia ni: Matamanio na Bida'a"

*Tazama: Tafsiri ssam'any 2/157.*

3- Amesema Al Imaam **Al baghawy** katika kuifasiri aya hiyo:

وَلا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ، أي: الطرق المختلفة التي عدا هذا الطريق، مثل اليهودية والنصرانية وسائر الملل، وقيل: الأهواء والبدع.
تفسير البغوي ٣/٢٠٥

"Na msifuate vijinjia, maana ya vijinjia: ni njia mbali mbali ambazo si hii njia (ya uislamu) , mfano uyahudi, unaswara, na mila zingine, na imesemwa kua maana yake: ni matamanio na bida'a".

*Tazama:Tafsiirul Baghawy 3/205.*

4-Amesema Al Allaamah **Alqurtubiyyu** Rahimahullaah-baada ya kuifasiri aya hiyo kwa hadithi ya Mtume Swalla Llaahu alaihi wasallam, iliyopokewa na Ibnu Mas'uud-:

وهذه السبل تعم اليهودية والنصرانية والمجوسية وسائر أهل الملل وأهل البدع والضلالات من أهل الأهواء والشذوذ في الفروع.
تفسير القرطبي ٧/١٣٨

"Na hivi vijinjia, vinaingia ndani yake uyahudi, na unaswara, na umajusi, na mila zingine na watu wa bida'a

na upotevu miongoni mwa watu wa matamanio, na shudhudhi kwenye mambo ya furu'I"

*Tazama:Tafsiri ya Qurtuby 7/138.*

5- Amesema **Asshaatwiby** Rahimahu Llaah- akifasiri neno:

ولا تتبعوا السبل

kwenye aya hiyo:

عام في كل ضال كان ضلاله كضلال الشرك أو النفاق ، أو كضلال الفرق المعدودة في الملة الإسلامية.

الاعتصام للشاطبي ١٠٨/١

"(Makusudio ya vijinjia hapo) inaenea kila mpotevu, kama vile upotevu wa shirki, au unafiki, au upotevu wa mapote yanayohesabiwa kua ni ya kiislamu"

*Tazama: Al I'itiswaam ya Asshaatwiby 1/108.*

6- Amesema Al Imaam **Ibnu Baazi** Alla amrehemu, akielezea makusudio ya vijinjia kwenye aya hiyo:

وقد دلت الأحاديث المرفوعة، والآثار عن الصحابة رضي الله عنهم، والتابعين لهم بإحسان، على أن السبل التي نهى الله عن اتباعها ، هي البدع والشبهات والشهوات المحرمة،

والمذاهب والنحل المنحرفة عن الحق، وسائر الأديان الباطلة.

مجموع فتاوى ابن باز ١/٢٣٤

"Na hakika hadithi ambazo ni mar'fuu'a, na aathaari kutoka kwa maswahaba Radhi za Alla ziwaendee na waliowafuata kwa wema zimeonyesha kua vinjia ambavyo Allah amekataza kuvifuata, ni bida'a, na shubuhaat, na matamanio haramu, na madhehebu na mila zilizopinda kutoka kwenye haki, na DINI zote za batili"

*Tazama: Majmu'u fatawa ya Ibnu Baaz 1/234.*

Kwa ufafanuzi wa wanachuoni hapo, tunaona wazi kua aya hiyo inafaa kutolea ushahidi wa kua vijinjia njia vinavyoitiwa na shetani ni dini batili ambapo wanaoitia kwenye vijinjia hivyo ni makafiri, na pia inafaa kutolea ushahidi kua ni bida'a ambao wanaoitia kwenye njia hizo ni watu wa bida'a.

Na ndio maana ninakunasihi Abdurrah'man utulie na usiwe na papara, na usipende kukimbilia kujibu bila kuwa na uhakika na unachotaka kuongea.

**Kosa la pili**(alilofanya Abdurrah'man katika ukosoaji wake) ni pale aliposema:

"Hadithi iko wazi, kwamba hawa wenye kulingania

katika moto wa jahannam ni nani? Waislamu au makafiri? Waislamu, Sasa wewe kusema kwamba wapo waislamu na wasiokua waislamu maneno haya umeyapata wapi na ni nani aliyetafsiri maneno hayo".

## UFAFANUZI NA JAWABU

**kwanza kabisa**: nimeelezea hapo juu kua hadithi hii niliitolea ushahidi ili kutilia mkazo kuingia baadhi ya waislamu(watu wa bida'a) katika watu wanaolingania kwenye vijinjia vya pembeni.

Lakini nikabainisha kua ibara nilizotumia zilikua za kimakosa( kama nilivyobainisha hapo juu) na kua Abdurrah'man alikua na haki ya kunikosoa kwenye hilo, ila kwenye ukosoaji wake amefanya makosa.

**Pili**: ni kweli kua mtiririko wa hadithi hii (ya Hudhaifa Radhi za Alla zimuendee) na kwa ufafanuzi wa wanachuoni wetu: inaonyesha kua waliyoongelewa hapo kwenye hadithi kua ni "walinganizi wa moto wa Jahannam" ni wale wanaojinasibisha na uislamu wanaoitia kwenye bida'a, kama ilivyokuja mwisho wa hadithi kua: "jitenge na hayo makundi yote"

**LAKINI LAZIMA UELEWE** kua katika hao watu wa bida'a wanao lingania watu kwenye bida'a zao: wako ambao bida'a zao zimewatoa katika uislam,japo wao wenyewe wanajihesabu waislamu, nao ni kama vile: walinganizi wa kiraafidhwa, walinganizi wa kijahmiyya, kama vile Jahmu bin Swafwan na wengineo, hawa wote wanaingia katika walinganizi wa motoni.

Kwa hiyo mtu anaweza kutolea hadithi hii kubainisha kua Jahmu bin Swafwaan, na yule kiongozi wa Hizbu LLaata, na walinganizi wote wa kiraafidhwa na kadhalika kua ni:

دعاة على أبواب جهنم

"**Ni walinganizi katika milango ya jahannam**"

kutokana na kua wao wanajinasibisha na Uislamu, na wanajidhihirisha kama mashekhe! Japo uhakika ni kua wao ni makafiri, na wanaingia katika mlango wa wanafiki kama tutakavyoona ufafanuzi wa Shaikhul Islaam hapo chini.

Na hii ni kama vile Imaam Ibnu Baaz Allah Amrehemu alipoelezea hadithi ya Iftiraaq baada ya

kuulizwa kama kundi la Ikhwaan Muslimuuna na Tabliigh yanaingia katika makundi sabini na mbili yaliopotea? Ambapo alijibu kua ndio yanaingia kisha akasema:

المراد بقوله"أمتي" أي: أمة الإجابة

"Makusudio ya kusema kwake: uma wangu, maana yake: umma uliokubali uislam"

Kisha akasema:

واثنتان وسبعون فرقة فيهم الكافر وفيهم العاصي وفيهم المبتدع أقسام

"Na makundi sabini na matatu (ya bida'a) wanapatikana ndani yake makafiri (ambao bida'a zao zimewatia kwenye ukafiri) na wako (watu wa bida'a) wenye maasi, na wako watu wa bida'a ( wasio fikia kiwango cha ukafiri)"

*Marejeo: kanda ya Shekhe ya darsa ya Al muntaqaa iliyokua inafanyika mjini Twaif, ilirekodiwa mwaka 1419.*

Maneno haya ya Imaam Ibnu Baaz yanabainisha kua wako watu wa bida'a ambao wanajinasibisha na Uislam, lakini kwa uhakika ni makafiri kwa Bida'a zao ( baada ya kuzingatiwa vidhibiti vya kukafirisha).

Na miongoni mwao ambao vidhibiti vya kukafirishwa vimetimia kwao: ni walinganizi wa Bida'a za Kijahmiyya, na Kiraafidhwa na nk, ambao hawa pamoja na kua Inawezekana wanaswali na

kufunga na nk, lakini kwa ulinganizi wao huo na itikadi zao ni makafiri, na hao ndio Imaam Ibnu Baazi aliowahesabu kua ni watu wa bida'a makafiri!

Na ufafanuzi huo wa Imaam Ibnu Baaz una mtangulizi katika salafy, naye ni Sheikhul Islaam Ibnu Taimiyya Allah amrehemu, ambapo katika kitabu chake Majmu'ul Fataawaa kuanzia 3/345: aliulizwa kuhusu hadithi ya kugawanyika Umma makundi sabini na matatu, na maana ya hayo makundi?

Ambapo alianza kubainisha maana ya Hadithi hiyo, kisha akataja baadhi ya makundi kama vile makhawariji, na mengineyo, kisha akataja khilafu ya wanachuoni katika kuyakufurisha baadhi ya makundi, kama vile Jahmiyya, na Raafidhwa, na mengineo, na kua wanaweza vipi kuingia katika hadithi ya kugawanyika Umma katika makundi sabini na matatu huku wamekufurishwa?

Sheikhul Islaam amelifafanua hili swala kuanzia 3/352 kwa kuelezea kua anayeingia kwenye ukafiri ( katika watu wa bida'a za ukafiri) akawa ana swali huyu

hawi isipokua mnafiki.Kisha akaeleza hali ya wanafiki na dalili zake, **halafu akasema:**

وَإِذَا كَانَ كَذَلِكَ فَأَهْلُ الْبِدَعِ فِيهِمْ الْمُنَافِقُ الزِّنْدِيقُ فَهَذَا كَافِرٌ وَيَكْثُرُ مِثْلُ هَذَا فِي الرَّافِضَةِ وَالْجَهْمِيَّة فَإِنَّ رُؤَسَاءَهُمْ كَانُوا مُنَافِقِينَ زَنَادِقَةً . وَأَوَّلُ مَنْ ابْتَدَعَ الرَّفْضَ كَانَ مُنَافِقًا . وَكَذَلِكَ التَّجَهُّمُ فَإِنَّ أَصْلَهُ زَنْدَقَةٌ وَنِفَاقٌ.

مجموع الفتاوى لابن تيمية ٣/٣٥٣.

"Na ikiwa ni hivyo: basi watu wa bida'a wako ndani yao mnafiki zindiki, huyu ni kafiri, na wanakua wengi hawa(wanafiki mazindiki makafiri) kwenye kundi la Rafidhwa na Jahmiyya, kwani viongozi wao(mashekhe wao na nk) walikua ni wanafiki mazindiki, na wakwanza kuzusha Uraafidwa alikua mnafiki, vile vile pote la Jahmiyya, hakika asili yake ni uzandiki na unafiki"

*Tazama: Majmu'ul fataawa ya Ibnu Taimiyya 3/353.*

Shaikhul Islaam hapa anaeleza kua watu wa bida'a, wakiwemo walinganizi wao ambao Mtume swalla Llaahu alaihi wasallam amewaita kua"Ni walinganizi walioko katika milango ya moto":

Wako miongoni mwao makafiri (ambao wanachukuliwa kama wanafiki), na hivyo mtu akikusudia kutoa hadithi hiyo kisha akasema kua:

miongoni mwa walinganizi hawa wa moto wa Jahannam wako waislam na wasio waislam, akikusudia watu wa bida'a ambao hawajakufuru na watu wa bida'a waliokufuru, kwa maana hii atakua kapatia.

Na kama atamaanisha waislamu (watu wa bida'a) na makafiri wa asili (mayahudi na manaswara na nk) basi atakua hajapatia (kama vile ibara ya maneno yangu ilivyokua inaeleweka hivyo kwa haraka haraka japo sijakusudia hilo kama nilivyobainisha hapo juu.)

**Kwa maana hiyo:** alitakikana Abdurrah'man aelezee swala hili kielimu zaidi, na si kueleza kiujumla kama hivyo, jambo ambalo linaweza kupelekea watu wakafahamu kua walinganizi wote wa bida'a wakiwemo Jaham bin Swafwan, Khomein, Nasru Sshaitwaan, na Huthi, na nk ni waislamu!

Pia wanaingia kwenye walinganizi walioko kwenye milango ya jahannam wote ambao asili yao na kizazi chao ni uislamu katika jamii za kiislamu

(husuusan waarabu), lakini wameuacha uislamu na kuitia kwenye ukafiri, kama vile kuitia kwenye Ilhadi( kutoamini uwepo dini) na wanaoitia kwenye madhehebu za kikafiri, kama vile dhehebu la ba'thy, na nk.

Na hii ni kutokana na kua Mtume Swalla LLaahu alaihi wasallam aliwasifu hao walinganizi wa Jahannam kua:

هم من جلدتنا ويتكلمون بألسنتنا

"wao ni katika ngozi yetu, na wanazungumza kwa lugha zetu"

Na baadhi ya wanachuoni walipokua wanawatahadharisha watu wa namna hiyo wametumia hadithi hiyo kuonyesha kua watu hao ni walinganizi walioko katika milango ya jahannam.

Na miongoni mwa wanachuoni hao ni Imaam Ibnu Baaz Allah amrehemu ambapo baada ya kuitaja hadithi hiyo (ya Hudhaifa Radhi za Allah zimuendee) katika moja ya maudhui zake **amesema**:

"فهذا الحديث العظيم الجليل يرشدك أيها المسلم إلى أن هؤلاء الدعاة اليوم، الذين يدعون

إلى أنواع من الباطل كالقومية العربية، والاشتراكية والرأسمالية الغاشمة، وإلى الخلاعة والحرية المطلقة وأنواع الفساد كلهم دعاة على أبواب جهنم"

مجموع الفتاوى لابن باز ١/٢٩٦.

"Hadithi hii tukufu, inakuongoza ewe muislamu, kujua kua hao walinganizi leo hii, ambao wanalingania kwenye aina mbali mbali za batili, kama vile uzalendo wa kiarabu,na ujamaa, na ubepari, na wenye kulingania kwenye ufisadi wa tabia na ufuska, na (pia wenye kulingania) kwenye uhuru usio na mipaka, na aina zote za ufisadi, WOTE HAO NI WALINGANIZI WAILIOKO KWENYE MILANGO YA JAHANNAM"

*Tazama: majmu'ul fatawa ya Ibnu baaz 1/296.*

Na inajulikana kua miongoni mwa wanaolingania kwenye mambo hayo wapo waliofikia daraja ya Ilhadi na kukufuru, kama vile watu wa Hizbul ba'thy na kadhalika.

Sina shaka ndugu msomaji kua maudhui hii imeeleweka vizuri, ila kuna nukta za msingi ambazo tutaziona kwenye MAKALA NAMBA NANE Inshaa Llah.

## IMEANDIKWA NA:

ABUU IBRAAHIIM IBNU AL IMAAM.

وفقه الله وغفر له ولوالديه ولجميع المسلمين.

١٤٣٨/٤/٢٠هـ